

**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI**

**THE HANSARD**

**Tuesday, 30<sup>th</sup> October, 2018**

*The House met at the County Assembly Chamber,  
Malindi Town, at 2.30 p.m.*

*[The Deputy Speaker (Hon. Kenga) in the Chair]*

**PRAYERS**

**MOTION**

GOVERNOR'S ADDRESS: EXPOSITION OF PUBLIC POLICY

THAT, Pursuant to the provisions of Standing Order o. 20(5), the thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of public policy contained in the First Address of the Second County Assembly by his Excellency, Amason Jeffah Kingi, E.G.H, The Governor, Kilifi County (Wednesday, 24<sup>th</sup> October, 2018), laid on the Table of this honourable House on Monday, 29<sup>th</sup> October, 2018.

*(Hon. Mwathethe on 30.10.2018)*

*(Resumption of debate interrupted on 30.10.2018)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Hon. Members, the Motion of the Second County Assembly speech by his Excellency, Amason Jeffah Kingi E.G.H, the Governor Kilifi County on Wednesday, October 24, 2018 had been moved by the Leader of Majority in the morning session and equally seconded by the Majority Whip during the same sitting. I now propose resumption of Debate.

For those Members who have not had an opportunity to make their contributions, make your requests. Yes hon. Chiriba.

**Hon. Chiriba:** Thank you Mr. Speaker, for giving me this opportunity to register my appreciation towards the Governor's speech. I was present during his Address and again I want to thank the Office of the Clerk for submitting copies of the same for our reference towards the Governor's Speech. The Speech that the Governor read is full of content and the issues that he mentioned in the docket of Education just to mention a few are very paramount.

In view of the same, I am seeing a responsibility to the House in the sense that... I believe the fulfillment of what is enshrined in the speech will put this county in a better position. Even the budgets that are ahead of us will be addressing or articulating the issues that were laid in this speech.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

I believe Pre- Primary Education is a very key issue as a foundation in our system of education. So, if the foundation is well set, you can be sure of success towards attaining the goal therein. We have a recent case of poor foundation of a one-storey building in the recent news here in Malindi which fell and caused even loss of lives outside other losses that we as Malindians faced. So, I believe if the Governor will stick to his utterances, to commitment and if this House will be supportive in defending the same, I believe tomorrow we will be talking of a change. So, I am in support of this Report. Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you very much hon. Member. We are now moving to hon. Stallone Humphrey Mkadi. Please proceed.

**Hon. Mkadi:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Kwanza, nimesimama pia kupongeza hotuba ya Gavana na niwapongeze wale wenzangu waliotangulia kuipongeza pale awali. Mimi nataka kuchukua nafasi hii kwanza kwa sababu mengi yameongewa, niongee kuhusiana na swala la michezo. Kweli Gavana ametambua kwamba kuna umuhimu wa michezo katika Kilifi Kaunti na hivyo akasema atachukua jukumu la kuboresha viwanja na hata kutengeza baadhi ya viwanja kama *stadiums*.

Ni vyema kwamba kutengeza uwanja huo itatusaidia sisi kama Kilifi Kaunti kupata hata mapato lakini mimi ningeomba kwamba sisi kama wabunge, kwa sababu kaunti jirani pale Mombasa miaka ile ya nyuma walijaribu kutambua talanta na hata kutengeza timu ya mpira ikiitwa Coast Stars. Timu hii ilikaribisha wachezaji wengi kutoka Kaunti tofauti tofauti na hivyo basi, Kaunti ya Mombasa ikawa imechukua mfano mzuri na timu nyingi pale zilijizatiti ili kupata nafasi kuingia katika ile timu ya Coast Stars.

Wengi wetu kama Kilifi Kaunti mwaka 2015 na 2016 tulishuhudia kwamba Kilifi Kaunti ilikuwa imeangazia mchezo wa mpira wa kandanda na ikawa wamekaribisha timu tofauti ili watengeze timu ya Kaunti. Mchuo huo ulikuwa pale Vipingo; timu zilitengezwa na zikapatikana timu mbili lakini timu hizo ziliishia hivyo hivyo, hatukujua kama mambo yalienda vipi. Mtazamo wangu mimi namuunga mkono Gavana lakini ningeomba sisi kama wabunge hasa hii Kamati yetu ya Michezo tukiongozwa na mwenyekiti wetu iwe tutaleta Hoja mbele hapa kwamba tutengeze timu tofauti tofauti tutambue vile vipawa vyenye watu wetu wa Kilifi Kaunti wako navyo na tuhakikishe tunavikuza kwanza ili kabla tutengeneze hivyo viwanja, hivyo vipawa tuwe tuko navyo.

Haitakuwa vizuri kwamba tutengeze viwanja na timu ambayo inawakilisha Kilifi Kaunti kwa kandanda hatuna. Ingekuwa bora kwanza tutengeze hizo timu; tutambue hivyo vipawa, tuwatayarisha, ndio ikifika wakati wa kutengeza viwanja, tuwe na watu ambao watavitumia vizuri vile viwanja. Hivyo basi itakuwa ni vizuri. Tumeona kwamba tunazo talanta hasa mchezo wa mpira. Tunao vijana ambao huko nyuma walicheza vizuri na saa hii hatuwaoni mahali; wengine wamepotea kwenye ulevi, wengine wamepotea kwenye anasa. Na hii sana sana inasababishwa na kwamba hata mtu akiwa mzuri katika mchezo fulani kwa sababu amekosa ajira, atapeana sana kipaumbele muda wake mwingi kutafuta kitu ambacho kitamsaidia kujikimu maishani kuliko kuendeleza ile talanta yake. Kaunti yetu inaweza kuwa na kazi tofauti tofauti ingekuwa vizuri wapewe vibarua ili waweze *ku-concentrate* na yale mambo ya michezo yao na yale mambo ya kukuza talanta zao ili waweze kuwa maarufu zaidi katika zile nyanja mbali mbali. Mimi nasimama kupongeza hotuba ya Gavana. Asanteni.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you. Hon. Members, let us now get the contributions of the Chair, Justice and Legal Affairs Scholastica Adit Oduor.

**Hon. (Ms.) Scholastica:** Thank you Mr. Speaker. I stand to congratulate our President of this County, His Excellency Jeffah Kingi, for a very brilliant speech that he gave the other day; that is last week on Wednesday. A lot has been said by my fellow hon. Members but what I want

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

to emphasize and thank the Governor through his speech is about the Education Sector. Some years back when I was still a young girl, because I came to Malindi so many years back we used to have a *shamba* around Kizingo. So, we could go there during school time in the evening just to go around and find what has been done at the *shamba*.

I used to find very small children there and I would ask them if they go to school and they would say '*kashomere*' by that time I did not know Giriama. So I use to wonder why these kids are saying '*kashomere*'. It is because maybe they were not going to school. But the Pre-Primary Education at least the Governor has highlighted on the County; we have ECDs around. We can see through our motions, the Governor was able to employ 666 teachers and mostly I want to thank the Governor so much because out of these 666 teachers, I believe 90 percent are the youths. As we can see now, the youths are not loitering around. At least they are somewhere; they have gotten employment, and at least we can see the cases of the youth unemployment are going down.

Secondly, there is a programme that the Governor wants to bring up. That is a Bill and that is why I stand as the Chairperson in the Legal Department because there are Bills and policies that are coming up especially the Bill on Pre-Primary Policy in the County and the Feeding programme. Actually, this is a very good Bill and I pray that all of us are going to embrace it and pass it. This Bill will help our children not to remain at home because some parents cannot even afford to cater for the meals for their kids. Once we have a programme in the schools, I can assure you no child will remain at home; every child will go to school. If I may ask you hon. Members, had you not gone through this, would you have been here today? No! So I support this so much and I ask all Members as I sit down that let us really appreciate our President for what he has done. Thank you so much Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Yes hon. Member for Matsangoni who is also the Chairperson for Water, Environment and Natural Resources.

**Hon. Hassan:** Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Nimesimama kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Gavana wetu wa Kilifi na kuipongeza hotuba yake. Mbali na mengi mazuri ambayo yamenukuliwa mimi kilichonifurahisha zaidi ni upande wa maji na mazingira. Kila mtu anaelewa ya kwamba maji ni uhai. Hii ni wazi kwamba kitengo cha Maji tumejitahidi kwa kiwango kikubwa katika kuendesha yale matatizo na mahitaji ya Kilifi kwa jumla. Kwa sababu ukiangalia hata nikinukuu kwamba tumeweza kuongeza yale mabwawa 65 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Vile vile, mwaka wa 2014 ilikuwa takwimu ni asilimia 48 za utoaji wa maji kwenye bomba na kufikia sasa, takwimu zinasema ni asilimia 65 hiyo inamaanisha kwamba Mungu akipenda kwa uwezo wake, tutakuwa tumefikia hatua kubwa sana labda kwa miaka miwili ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa mazingira, kilichonifurahisha zaidi ni kuna mpango wa kutafuta kampuni ambayo itabadilisha hizi takataka na kufanywa mambo mengine kama uzalishaji wa mbolea, umeme na vyenginevyo. Mbali na kazi hizo, itakuwa ni njia moja ya kutupatia ajira na ombi langu kubwa kwa Waheshimiwa ni kwamba hii hoja itakapokuja wakati huo, maana iko njiani, nawaomba kwa unyenyekevu kabisa tuiunge mkono ili na sisi tuingie katika viwango vya kimataifa. Kwa hayo machache, nimeshukuru na ninaunga mkono wenzangu. Asanteni sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you. For those Members who would wish to make their contributions, please make your requests. Hon. (Ms.) Koki.

**Hon. (Ms.) Koki:** Thank you Mr. Speaker. I stand to congratulate our Governor on a very wonderful speech that he gave us the other day and he mentioned something that is very close to my heart on women and youth empowerment. This is what I do on a daily basis and if I

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

can mention what he said was construction of youth empowerment centres. For women, he also mentioned something about empowering and value addition which will be undertaken in all the wards within the County. This is something that we should all support because we know empowering a woman is empowering the nation. Our women are seated in their homes while they can do something for their daily bread.

I urge Members, when this programme starts in the Department of Gender, Social Services and Culture, we should support and make sure no woman is left behind. The empowerment programme will also help in developing our county. Thank you.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): The Leader of Minority, please make your contributions.

**The Leader of Minority** (Hon. Matsaki): Asante sana mhesimiwa Spika. Mimi nitaongea kwa uchache kwa sababa mengi yamezungumzwa na msawa huu hauna *vote*, ni kuzungumza yale unajisikia. Kwanza, nataka nishukuru kwa vile leo tumeanza kujadili hotuba ya Gavana na nikiwa kiongozi wa wachache, siko hapa kupinga kila kitu ambacho kinaletwa hapa lakini nataka niseme naunga mkono hotuba hii. Mbali na uongozi, alitambua Bunge kama kiungo muhimu kwa maswala ya ugatuzi kwa sababu kama si Bunge, mambo mengi ya ugatuzi hayangekuwa vile yanastahili.

Pili, Gavana alitambua bila ushuru wa kutosha si rahisi kufanya miradi yetu ya wananchi kule mashinani na ndio sababu kipindi kilichopita na hata sasa tukiongea kuhusu Rain Drops, aliona hawa akiwaacha kama vile walivyo, basi sisi kama kaunti tutakosa pesa za ushuru na ndio sababu akaweka wale maofisaa wetu ili waangalie kama hawa watu wanafanya kazi kikamilifu ama namna gani. Katika hali hiyo, ushuru ukaanza kuongezeka lakini tunataka tufahamu kama ushuru unaongezeka, unaongezeka kwa hazina zetu ama inaongezeka vipi? Ninamshukuru kwa sababu yeye mwenyewe amejua kuna mahali fulani kuna matatizo.

Jambo lengine ambalo nataka niongee kuhusu na mambo ya *Disaster Management*. Nataka niseme Kilifi Kaunti tumekuwa na majanga mengi sana hasa ya mafuriko, kwengine moto ni hali ya kutaka kujipanga na vile alijieleza katika hotuba yake, ni tuwasaidie wale ambao wamepatwa na majanga haya kama kuwapelekea chakula. Hizi huwa ni huduma muhimu sana kama vile kuwapelekea blanketi wakati wa baridi. Serikali inayotambua shida za watu wake huwa ni serikali ambayo iko imara. Hapo ningetaka kumshukuru.

La mwisho ni kwamba upande wa elimu kusema kweli tumejaribu. Kutoka kipindi cha kwanza, zile shule za chekechea na kuwaajiri *caregivers*, madawati na pia imetupeleka mbele zaidi na maziwa. Unajua watoto wakiwa wanapata vile vitu vidogo huwa ni vitu muhimu sana. Mara nyingi, watoto wetu huwa wakitoka asubuhi mara nyingine pale nyumbani huwa na changamoto na hukosa hata kikombe cha uji. Kwa hivyo, mimi nataka nishukuru kwa sababu haya ni mambo ambayo yamefanyika.

Pia, nisingetaka nisahau kuhusu *Scholarship* ambayo inatolewa na serikali na tunaisimamia kule mashinani. Kusema kweli, inasaidia pakubwa kwa sababu wale watoto ambao wametoka katika familia maskini wamesaidika na hii ni kwa sababu ijapo bado hatujafikia pale, tunataka lakini inasaidia watoto na karo na inapendeza. Japo yako mengi ambayo yanatajikana yafanywe, mimi nisingetaka niongee sana kwa sababu kuna wengi hawajaongea lakini kwa ujumla, nataka niunge mkono hotuba ya Gavana. Pale ambapo kumeenda chini kwa sababu mimi mara nyingi husema mwanadamu si kamili, sio kila kitu wewe utasema ni kizuri lakini lazima tuanzie mahali. Kwa hivyo, pale mahali tumeanzia mimi nasema nashukuru na yale ambayo pengine yanaonekana hayakufanyika vizuri pia ni ile hali ya kupeana moyo ili yeye naye ajaribu ni wapi anaweza akatilia mkazo. Kwa hayo machache, mimi nimesimama kuunga mkono hotuba ya Gavana.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you, hon. Members that was the Leader of Minority making his contributions regarding the Governor's address. In my request list I have one Member who has requested to speak.

Therefore, if you are not going to make your request then we shall be forced to adjourn once he is through with his contributions. So, please for those Members who have not contributed and would wish to contribute to the Governor's Address, this is your opportunity to make your request. I am also seeing Members who have contributed in the morning sitting. Guided by Standing Order No. 78, we cannot have an opportunity to speak twice to the Motion that we are now making contributions.

Now, for those who have not made their contributions they have an opportunity. So the Member for Rabai Kisurutini hon. Cantona (Mae) please proceed.

**Hon. Mae:** Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi nasimama kuunga mkono hotuba hii ijapokuwa sio kila kitu kilicho humu tunastahili kukishabikia. Kwa sababu sitagusia kila kitengo lakini mimi nitaenda moja kwa moja kwenye swala la Ardhi.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka wakati wa nyuma, wakati serikali ya Kenya ilipovamiwa na majambazi tunaowaita Al-shabaab na kwa kuwa swala la usalama liko katika mikono ya serikali kuu, Rais alijizatiti kupiga vita kuhakikisha usalama unapatikana kwa sababu kikatiba uko mikononi mwake. Sisi hapa Kilifi tumeona upande wa ardhi kuna hati miliki zimepeanwa na mashamba yamepimwa. Kwa hivyo, tunashukuru na tunampa kongole mheshimiwa Gavana. Lakini hao mabepari na wanyakuzi wanapokuja kunyakua ardhi zetu hapa Kilifi ni nani anayesimama kidete kumlinda mtu wa Kilifi? Je, ni Gavana ama ni mwakilishi wa Wodi? Mimi nilitarajia Gavana aligusie hilo swala na ametuwekea mikakati gani kama wakaazi wa Kilifi.

Juzi ndugu yetu mheshimiwa Kazungu Dele alipatwa na changamoto. Na changamoto hizo zikaonekana ni kama ni za watu wa Sabaki, na pia zikaonekana ni changamoto za mheshimiwa Dele. Lakini je, kama Rais wa jimbo na tunavamiwa kila siku nilitarajia Gavana angegusia hilo kwa sababu, sidhani kama unapoenda Kaunti zengine kama mtu wa Kilifi; unapoenda Nyeri, bonde la ufa, Murang'a sidhani kama kuna watu kutoka huku wanakwenda kule kuingia na kunyakuwa ardhi, iwe na hati miliki isiwe na hati miliki. Lakini kilifi na Pwani kwa ujumla imekuwa ni mahali pa kuchezea. Saa hivi mpaka Wa-Hindi pia wananyakua ardhi; ni mkaazi gani wa Kilifi ana ardhi Bombay ama alikunyakua ardhi kule?

Mheshimiwa Spika, swala hili juzi lilimwingiza mwenzetu kizimbani. Mimi swala kama hili lilinifanya nikashindwa kulala kwetu nyumbani miezi miwili kwa sababu kulikuwa na ubomoaji kama huo na tulivyosimama pale, ikasemekana mimi nimechochea na polisi wakawa wananiandama. Ukumbuke usipolala nyumbani ina maana kuwa utumie mfuko wako kulala sehemu tofauti. Mheshimiwa Spika, ijapokuwa maneno haya ya Gavana yalistahili kuandikwa kwa wino wa dhahabu kwa mpangilio uliopangwa, lakini kuna vipengele vingi vilivachwa wazi na sisi tunategemea endapo tutapata fursa nyengine ya kukutana na Gavana basi atuambie yeye kama Rais wa jimbo, atapanga vipi kupambana na hawa mabepari. Asanteni sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you very much. Let us go to the hon. Member Jana Tsuma Jana. Just make your contributions.

**Hon. Jana:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa kuniona. Mimi nami nasimama kuunga mkono hotuba hii ya mtukufu mstahiki Gavana wetu ambaye tunampenda. Mimi hasa nimefurahishwa na hili jambo la ukulima, kwa sababu haya yote ambayo yameweza kuongewa yatawezekana basi tunaamini vijana wetu wataweza kujiajiri mashinani ili kusudi kupunguza ukosefu wa kazi.

Kwa hivyo, ninasema ninaiunga mkono kwa dhati na kusema kwamba hii ni Hotuba ya maana na inastahili. Asante sana Bw. Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you for making your contributions. We are now moving to the Member for Ganze Ward, hon. Benson Chengo. Please proceed.

**Hon. Chengo:** Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama pia mimi kuunga mkono hotuba ambayo Gavana wetu aliitoa juma lililopita. Ilikuwa hotuba nzuri na ninaamini kwamba kama itafuatwa vile ilivyo, wana Kilifi tutafurahia. Labda tu kwamba kuna moja ambalo nataka kuzungumzia; juzi nilikuwa *Mashujaa day* kule nyumbani Ganze na ile hotuba ya Gavana basi niliona ni kama iliniletea aibu kwa sababau wananchi wangu walisema haikuleta mradi wowote mzuri eneo hilo. Lakini utakuta kwamba miradi yote ililenga maeneo ya miji ama huko kwengine ndio maana wale wakaazi wakawa wanasema huyo *Sub-County administrator* afadhali akae kwa sababu hakuna mradi wowote wa kujivunia.

Kwa hivyo, ombi langu ni kwamba nafikiria kama itawezekana, wakati mwengine kule mashinani kufikiriwe kwa sababu tuko na tunaishi kule kule. Asante kwa hayo machache mheshimiwa Spika na nasimama kuunga mkono.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Member for Marafa hon. Renson Kambi Karisa, please proceed.

**Hon. Karisa:** Asante. Kama unavyojua, wakati huu ni wakati wa mabadiliko. Usipokubali kubadilika, mabadiliko yatakubadilisha. Maono ambayo Gavana ameweza kunukuu hapa, naona kile kilichobaki ni jukumu la waheshimiwa hapa Bunge na Kamati tofauti tofauti kwa sababu nimeona amegusia Kamati zote katika ukulima, uchukuzi, mambo ya afya na mengi mengine. Iliyobaki ni jukumu la sisi waheshimiwa pamoja na mawaziri tunatia bidii kuhakikisha kwamba zile ndoto zilizotajwa hapa na Gavana zimetimia ili mwananchi akanufaike. Nimesimama kuunga mkono hotuba ya Gavana kwa dhati ili kuona kwamba matarajio ya wananchi yamefanikishwa vizuri mashinani ni sisi tupate kutambua ni wizara gani tutazipa kipao mbele ili kuwasaidia wananchi.

Ukiangalia Wizara nyengine ni kama zimebebwana... (*inaudible*). Kwa mfano, tuchukulie wizara ya Kilimo; ikiwa ukulima unafanya vizuri, wizara ya Viwanda pia itafanya vizuri. Kwa hivyo, ni jukumu letu sisi kama waheshimiwa tuangazie zile wizara zinazoweza kusaidia wananchi zaidi na kufanikisha malengo ya Gavana.

Tukiangalia wizara ya Kilimo kuna baadhi ya miradi ambayo imefadhiliwa hata imebaki tu serikali yetu iwekeze michango yetu ili tusikose miradi hiyo. Iwapo Kamati na mawaziri watashikana na kuhakikisha wanatekeleza maono ya Gavana, basi tutaweza kufaulu katika serikali yetu ya Kilifi. Nasimama kuunga mkono hotuba hii ya Gavana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you. The Member for KADU-ASILI, hon. Mwarandu, would you wish to contribute?

**Hon. Mwarandu:** Asante sana Mheshimwa Spika. Kwanza kabla sijachangia, naomba kujua kama ni sawa kuendelea kama Bunge halina *quorum*.

*(The Clerk-at-the-Table consulted with the Deputy Speaker)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): There is quorum hon. Member.

**Hon. Mwarandu:** Kwa vile mheshimiwa Messo ameingia, *quorum* imefika. Nitafwata mwelekeo tofauti na wenzangu. Kulingana na mimi, hotuba ya Bw. Gavana ni kama kuvaa suti nzuri nje, ndani chupi imepasuka; kwa sababu maneno aliyotumia ni mazuri yanapendeza lakini tukielekea katika Idara ya (ICT) Teknolojia sioni kama Kilifi Kaunti ina malengo kuhusiana na

tekinolojia. Idara ya ICT inapaswa kuwa idara kubwa zaidi kuliko idara zingine zozote kwa sababu inachukua mkondo wa idara zote zinazoendeshwa hapa Kilifi Kaunti.

Yale Bw. Gavana ameelezea machache ambayo kwangu mimi sioni kama yamefaidisha Kaunti hii. Ameelezea kuhusu *road area network* na *electronic data management system*. Hivi ni vitu ambavyo vinafaidi watu wachache. Kwangu mimi, teknolojia ni kitu ambacho vijana wakielimishwa vizuri kama vile kuna huu msembo ambao unaitwa ajira au *digital*. Mambo kama hayo yakifunzwa vizuri yatafaidi vijana wa Kaunti hii. Kwa maoni yangu ni kama tumepakwa mafuta na mgogo wa chupa ilhali mafuta yenyewe yako ndani ya chupa. Kwa hayo machache, napinga hotuba.

**The Deputy Speaker** (Hon. Kenga): Thank you hon. Member for your contribution. The Motion as moved and seconded has been debated by the Members who have made their contribution.

*(Question put and agreed to)*

Hon. Members, we have come to the end of our debate of the public policy contained in the Governor's Address. I now urge the respective Committees of this House to follow up with the County Executive Departments on the various legislative proposals and programmes contained herein and ensure they are submitted promptly so that the legislative agenda of this House can take its course.

### ADJOURNMENT

There being no other Business on the Order Paper, this House stands adjourned until tomorrow, Wednesday, at 2:30 p.m. Thank you. God bless you.

**The House rose 3:43 p.m.**